

## **KAMPENI YA SIKU 16 ZA KUPINGA UKATILI WA KIJINSIA NA UKATILI DHIDI YA WATOTO**

### **1.0. UTANGULIZI – CHIMBUKO LA SIKU 16 ZA KUPINGA UKATILI**

Siku 16 za kupinga ukatili dhidi ya Wanawake ni kampeni kabambe ya kimataifa ya kupinga ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto. Chimbuko la siku hiyo ni mauaji ya kikatili ya wanawake watatu (3) wanaharakati wa kupinga ukatili dhidi ya wanawake yaliyofanywa na utawala wa kidikteta wa Jamhuri ya Dominica tarehe 25 Novemba, 1960. Ilipofika Novemba 25 mwaka 1999, Baraza Kuu la Usalama la Umoja wa Mataifa lilitenga siku hii kuwa ni siku ya Kimataifa ya kupinga Ukatili dhidi ya wanawake ikiwa ni sehemu ya kuenzi harakati za kupinga ukatili huo na kuimarisha upatikanaji wa Haki za Binadamu. Kampeni hii huanza tarehe 25 Novemba hadi 10 Desemba ya kila mwaka kwa siku 16. Kampeni nyingine zinazoambatana na siku 16 za kupinga ukatili ni Siku ya Kimataifa ya Watetezi wa Haki za Wanawake (Novemba 29) na Siku ya kukumbuka mauaji ya kikatili ya Montreal, Canada (Desemba 6, 1989) ambapo wanawake 14 waliuawa na mtu aliyekuwa anawachukia wanawake.

### **2.0. UKATILI WA KIJINSIA NA UJKATILI DHIDI YA WATOTO NCHINI**

Ukatili ni matumizi ya makusudi ya nguvu au vitisho vinavyofanywa na mtu au kikundi cha watu vinavyoweza kumsababishia mtu madhara ya kimwili, kiafya na kisaikolojia. Vitendo vya ukatili hufanywa zaidi kwa kundi la wanawake na watoto. Kwa mijibu wa taarifa za Jeshi la Polisi nchini kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021 jumla ya watu 29,373 walifanyiwa ukatili wa kijinsia ikilinganishwa na watu 42,414 kipindi kama hicho cha mwaka 2020. Matukio ya **ukatili wa kijinsia** yaliyoongoza kwa idadi kubwa ya waathirika ni ubakaji (6,305), shambulio (5751) na lugha ya matusi (3,015). Matukio ya ukatili wa kijinsia yalipungua na kufikia 13,041 kwa kipindi cha 2020/21. Mikoa ya kipolisi iliyoongoza kwa matukio ya ukatili wa kijinsia ni Arusha (4,320), Ilala (2,680), Tanga (2,257), Kinondoni (1,985) na Rukwa (1,575).

Kwa upande wa **watoto** katika kipindi cha Januari - Desemba, 2021, jumla ya matukio 11,499 ya ukatili kwa watoto yaliripotiwa ikilinganishwa na matukio 15,870 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020. Huu ni upungufu wa matukio 4,371 kwa kipindi cha 2020/21. Mikoa ya kipolisi iliyoongoza ilikuwa ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na Ilala (489). Makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ya matukio ya ukatili kwa watoto ni Kubaka (5,899), Kumpa mimba mwanafunzi (1,677) na Kulawiti (1,114).

### **3.0. URATIBU WA KAMPENI**

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ina jukumu la kisera la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala ya Haki za Watoto, Usawa wa Kijinsia na kuratibu afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kushirikisha Wadau nchini. Katika kampeni ya Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya Watoto, Wizara kwa kushirikiana na Wadau imepanga kuendesha kampeni mbalimbali za kutokomeza vitendo vya ukatili ambapo uzinduzi utafanyika tarehe 25 Novemba na kuendelea na kampeni hadi tarehe 10 Desemba, 2022. Kampeni zitafanyika katika ngazi zote kuanzia Taifa, Mikoa, Wilaya, Kata na ngazi za Vijiji/Mitaa kulingana na mazingira na taratibu za maeneo husika. Aidha, Wizara inasisitiza kufanyika kwa matukio ya kimkakati katika kampeni hizo kama yafuatayo;

- i. Kutoa tamko la kitaifa la Wizara kuhusu kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto kwa waandishi wa habari
- ii. Uzinduzi wa kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia tarehe 25 Novemba, 2022 katika ngazi ya Taifa, Mikoa, Wilaya, Kata, Vijiji/Mitaa kwa maandamano na mabango yenye jumbe za kupinga ukatili kwa kushirikisha makundi yote katika jamii (Watoto, Wanawake, Wazee, wenye ulemavu), viongozi wa dini, polisi, wasimamizi wa sheria, vikundi vya hamasa – SMAUJATA, viongozi wa mila n.k. Maandamano yatahitimishwa kwa maelezo ya viongozi katika maeneo husika kuhusu mbinu na mikakati ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto katika maeneo yao.

- iii. Viongozi, wataalamu na vikundi vya hamasa kuratibu na kusimamia mijadala/makongamano katika ngazi zote ikiwa pamoja na kwenye nyumba za ibada, vijiwe vya boda boda, masokoni, mashuleni na vyuoni (kutoa elimu na kuanzisha madawati ya ulinzi na usalama wa watoto), na kufanya kampeni maeneo yote yenye mikusanyiko ya watu ili kujadili na kuweka maazimio ya pamoja katika kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia na watoto katika ngazi ya jamii. Matukio haya yafanyike baada ya uzinduzi hadi tarehe 10 Desemba, 2022.
- iv. Kuainisha baadhi ya viongozi (serikali, dini na kimila), wataalamu na watu wenye ushawishi katika jamii kwenda katika vyombo vya habari; luinga na radio hasa radio za kijamii kuzungumzia vitendo vya ukatili wa kijinsia na hasa ukatili dhidi ya watoto katika kipindi chote cha siku 16 za kupinga ukatili. (maelezo yenye kujenga uelewa kuhusu ukatili yameambatishwa)